

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA
MAKUNDI MAALUM

Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346
Nukushi: +255 (026) 2963348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz
Tovuti: www.jamii.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P 573,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI YA KITAIFA YA KURATIBU AFUA ZA
KUDHIBITI NA KUZUIA WATOTO KUISHI NA KUFANYA KAZI MITAANI.

DODOMA, 3 AGOSTI, 2024

Nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na tatizo la Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mitaani katika maeneo mbalimbali yenye shughuli nyingi za kiuchumi. Watoto hao wamekuwa wakitumikishwa katika kazi ndogondogo, kuomba omba mitaani na kusababisha kukosa haki zao za msingi zikiwemo elimu, matunzo, malazi, ulinzi na usalama. Nikiwa Waziri mwenye dhamana na watoto, nimeteua Kamati Maalum ya kushughulikia tatizo hilo Kitaifa ikiwa ni kuunganisha nguvu za pamoja na Wizara za Kisekta, Taasisi, Wadau wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kukabiliana na tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Kamati hiyo itakuwa na majukumu ya kufanya tathmini ya ukubwa wa tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani nchini; kuandaa mpango na mwelekeo (roadmap) wa **utekelezaji wa afua za kuzuia tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani**; kushirikiana na Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto nchini; Mamlaka nyingine za Serikali na kuhakikisha watoto hao wanaunganishwa na huduma mbalimbali za kijamii.

Wajumbe walioteuliwa kuunda Kamati hiyo ni:-

NA	JINA LA MJUMBE	TAASISI	NAFASI
1.	Dkt. Nandera E. Mhando	Kamishna - Ustawi wa Jamii (WMJJWMM)	Mwenyekiti
2.	Mussa Mgata	Mkurugenzi Railway Children Africa (RCA)	Mwenyekiti Mwenza
3.	Godwin J. Semunyu	Benki ya NBC	Makamu Mwenyekiti

NA	JINA LA MJUMBE	TAASISI	NAFASI
4.	Subisya Kabuje	Mkurugenzi Msaidizi - Ustawi wa Jamii (OR-TAMISEMI)	Katibu
5.	Baraka P. Makona	Kamishna wa Ustawi wa Jamii Msaidizi (WMJJWMM)	Katibu Mwenza
6.	ACP. Faidha Y. Sulemani	Dawati La Jinsia Na Watoto Taifa (IGP)	Mjumbe
7.	Bi. Tulia Msemwa	Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu	Mjumbe
8.	Gerald W. George	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mjumbe
9.	Sarah Felix Ndaba	Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulenya nchini.	Mjumbe
10.	Rukia Kibwana	Mamlaka ya Kudhibiti Usafiri Ardhini	Mjumbe
11.	Insp. Kato Mdathiru	Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam	Mjumbe
12.	Elisha Nyamala	Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam	Mjumbe
13.	Josephine Komngazi	Benki ya NMB PLC	Mjumbe
14.	Florian Fanuel	Mkurugenzi SOS Village	Mjumbe
15.	Levina Kikoyo	Mkurugenzi Mtendaji - PACT Tanzania	Mjumbe
16.	Wallace Karia	Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF)	Mjumbe

Kufuatia uteuzi huo, Kamati hii itadumu kwa muda wa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 1 Agosti, 2024 hadi 31 Julai, 2027.

Dkt. Dorothy Gwaiima (Mb)
**WAZIRI WA *Dwajina* JAMII, JINSIA,
 WANAWA MAALUM.**